# MPENI BWANA UTUKUFU NA NGUVU

Zab. 96 : 1, 3-5, 7-10 (K) 7

**Wimbo wa Katikati**
**Jumapili ya 29, Mwaka A**

Rogers K.J
2006
Dodoma




1. Mwimbieni Bwana wimbo mpya, Mwimbieni Bwana nchi yote//
   Wahubirini mataifa habari za utukufu wake; Na watu wote habari za maajabu yake.

2. Kwa kuwa Bwana ni mkuu mwenye kusifiwa sana, Na wa kuhofiwa kuliko miungu yote//
   Maana miungu yote ya watu si kitu; Lakini Bwana ndiye aliyezifanya mbingu.

3. Mpeni Bwana enyi jamaa za watu, Mpeni Bwana utukufu na nguvu//
   Mpeni bwana utukufu wa jina lake; Leteni sadaka mkaziingie nyua zake.

4. Mwabuduni Bwana kwa uzuri wa utakatifu, Tetemekeni mbele zake nchi yote//
   Semeni katika mataifa Mungu ni mfalme; Atawahukumu watu kwa adili.